

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI

19 JUNI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA HAMSINI – TAREHE 19 JUNI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

**651. MHESHIMIWA ANGELINA ADAM
MALEMBEKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, lini Serikali itaongeza Mafao kwa Askari Wastaafu.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

652. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kutatua changamoto ya Vifaa Tiba katika Hospitali za Wilaya zinazojengwa.

653. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni haja ya kuigawa Shule ya Msingi Mwanhuzi kwa kuwa Shule hiyo ina takribani Wanafunzi 1400.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

654. MHESHIMIWA AGNESTA LAMBERT KAIZA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, kwa nini Serikali isisamehe kodi na kuondoa baadhi ya Tozo katika Sekta ya Elimu na Afya ili kuvutia Taasisi Binafsi.

655. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali ipo tayari kuiwekea SUMA JKT mazingira rafiki ili iweze kukopa na kutekeleza miradi yake kwa wakati.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

656. MHESHIMIWA GEOFFREY IDELPHONCE MWAMBE (MASASI MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa kilomita 1000 za Reli ya *Standard Gauge* kati ya Mtwara - Mbamba Bay na Songea - Ludewa.

657. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya ujenzi wa barabara ya Karatu - Mbulu hadi Singida Kilomita 190.

658. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:

Je, lini Serikali itaendeleza Barabara ya Mpanda - Kahama ili ifike Ulyankulu - Urambo - Ussoke - Tutuo - Sikonge hadi Mbeya.

WIZARA YA NISHATI:

659. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini zoezi la kufikisha umeme katika Vitongoji, Vijiji na Mitaa ambayo haina umeme litakamilika Wilayani Kakonko.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

660. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Wanafunzi wote waliomaliza Kidato cha Sita wanapata Mkopo wa Elimu ya Juu.

WIZARA YA MAJI:

661. MHESHIMIWA VENANT DAUD PROTAS (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, nini mpango wa kuweka miundombinu ya kuhifadhi maji ya mvua badala ya kusababisha mafuriko Kata za Loya na Miswaki.

WIZARA YA MADINI:

662. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, kuna mkakati gani wa kutatua kero zinazowakabili Wachimbaji na Wasafirishaji wadogo wa dhahabu Mgodu wa Kebaga.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

663. MHESHIMIWA NORAH WAZIRI MZERU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mpango gani wa kuwawezesha Wadau wa Michezo kuwekeza katika kuzalisha Vipaji vya Michezo hasa mpira wa miguu.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2022 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
19 JUNI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**